**HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. CHIKU A. GALLAWA MKUU WA MKOA WA SONGWE KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO CHA WADAU WA AFYA MKOA WA SONGWE UKUMBI WA CHUO CHA UUGUZI MWAMBANI ,WILAYANI SONGWE TAREHE 14 - 15/JULAI/2018:**

**Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe,**

**Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,**

**Waheshimiwa wenyeviti wa Halmashauri,**

**Viongozi kutoka Idara mbalimbali Mkoa wa Songwe,**

**Makatibu Tawala wa Wilaya,**

**Wakurugenzi watendaji wa Halmashauri za Wilaya,**

**Wakuu wa Idara,**

**Viongozi mbalimbali kutoka Halmashauri,**

**Viongozi wa dini,**

**Asasi zisizo za kiserikali,**

**Waandishi wa habari,**

**Wageni Waalikwa wote,**

**Mabibi na mabwana wote mliofika hapa,**

Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa kunipa heshima na jukumu hili la kuwa mgeni rasmi na mwenyekiti wa kikao hiki cha wadau wa Afya Mkoa wa Songwe.

Ninaamini nafasi hii sijapewa kama Mkuu wa Mkoa peke yake, bali pia mmezingatia kuwa mimi kama kiongozi miongoni mwa walengwa wa kikao hiki nina nafasi kubwa katika kushirikiana nanyi kutafakari mafanikio, matatizo na changamoto za kimaendeleo zinazoikabili sekta ya Afya hapa Nchini na hususani Mkoa wa Songwe.

Ninapenda pia kuwapongezeni kutokana na maandalizi makubwa yaliyofanyika mpaka kufikia kufanyika kwa kikao hiki, vilevile ninawashukuru wajumbe wote mlioitikia wito na kufika kwenye kikao hiki muhimu, hii inadhihirisha jinsi ambavyo mmezipa kipaumbele huduma za Afya katika Mkoa wetu.

**Ndugu Washiriki**: Huduma za afya na ustawi wa jamii katika Mkoa wetu zimepata mafanikio kiasi kutokana na jitihada zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo. Katika kipindi cha miaka 2 tangu kuanza kwa Mkoa wetu, mwezi Januari, 2016 umepata mafanikio kwenye maeneo yafuatayo:

1. Vituo vya Kutolea huduma za afya katika Mkoa wa Songwe vimeongezeka kutoka vituo **172** hadi kufikia vituo **182**.

2. Kuanza kwa **huduma za Upasuaji wa dharura** kwa akina mama wajawazito katika Vituo vya afya vya **Tunduma** na **Kamsamba** lengo ikiwa ni kupunguza na kutokomeza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga.

3. Maambukizi ya UKIMWI yamepungua kutoka 9.1% mwaka 2011/2012 hadi kufikia 5.8% mwaka 2016/2017

4. Kupungua kwa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kutoka 3.6% hadi 2.7%

5. Kiwango cha watoto waliochanjwa kimepanda kutoka 89% hadi kufikia 98% kwa mwaka 2017.

6. Idadi ya kaya ambazo zimejiunga na mfuko wa afya ya jamii zimeongezeka kutoka 66% hadi 76%

7. Upatikanaji wa dawa muhimu kwenye vituo vya tiba umeongezeka kutoka 70% hadi 94%.

8. Vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kutoka 37 (124/100,000) hadi kufikia 27 (81/100,000)

9. Wakinamama wanaojifungulia kwenye vituo vya huduma za afya wameongezeka kutoka 58% hadi 76%

**Ndugu Washiriki:** Pamoja na mafanikio hayo , bado tunakabiliwa na changamoto mbalimbali za utoaji wa huduma za afya.
Baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta ya afya ni:

1. Uhaba wa vituo vya kutolea huduma za Afya, mf. Kati ya Halmashauri 5 za Mkoa wetu, ni Halmashauri 2 tu (Mbozi na Ileje) zenye Hospitali za Halmashauri, bado halmashauri 3 hazina hospitali za Wilaya. Vituo vya afya vinavyomilikiwa na serikali ni 8 tu kati ya vituo 94 vinavyohitajika ili kila kata iwe na kituo cha Afya.
2. Upungufu mkubwa wa watumishi wa afya kwani watumishi waliopo ni 997 sawa na (39.53%) kati ya watumishi 2,522 wanaohitajika, hivyo kufanya kuwa na upungufu wa watumishi 1,525 sawa na (60.46%).

3. Upungufu mkubwa wa magari ya kubebea wagonjwa kwani yaliyopo kwa Mkoa mzima ni Magari(*Ambulances*) 6 tu kati ya magari 13 yanayohitajika

4. Uwepo wa magonjwa ya kuambukiza, kama vile Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu, japo inaonesha kuna kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya Malaria (kutoka 4%-2%) na VVU,(kutoka 9.1%-5.8%) kwa kipindi cha kuanzia 2016/2017 hata hivyo kiwango cha maambukizi ya Kifua Kikuu kimekuwa kikiongezeka. Kwa mwaka 2017, Wagonjwa walioibuliwa kwa kipindi hicho ni 1,017.
5. Uwepo wa magonjwa yatokanayo na uchafu wa mazingira kama Kipindupindu na magonjwa mengine ya Kuhara.
6. Kutokuwa na stoo ya chanjo ya Mkoa ( Regional Vaccine Store)

7. Uwepo wa ugonjwa wa ebola katika nchi jirani ambayo tuna muingiliano nayo mkubwa wa shughuli za kiuchumi na kijamii hivyo hivyo kupelekea kuwa na tishio la ugonjwa huo kuenezwa kuingia nchini mwetu.

Ndugu washiriki: Ninapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru kwa dhati Wadau na mashirika mbalimbali tunayofanya nayo kazi katika sekta ya afya ndani ya Mkoa wetu, wadau hawa na mashirika haya yametoa mchango mkubwa sana katika kuboresha huduma za Afya katika Mkoa wa Songwe. Baadhi yao ni shirika la kuhudumia watoto ulimwenguni ( UNICEF),shirika HJFMRI chini ya program ya Walter Reed Programme-Tanzania, JHIPIEGO, JSI, PSI, CARITAS, IRDO, AFRICARE Save the Children na ADP. Shughuli zinazofanywa na mashirika na taasisi hizi zimechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio

yaliyopatikana. Ninazidi kuwasihi wadau waendelee kushirikiana na Sekretarieti ya mkoa, pamoja na halmashauri na wananchi kwa ujumla kuendelea kuboresha hali za afya za wananchi.

**MIPANGO NA MIKAKATI YA SERIKALI**

**Ndugu washiriki:** Katika kukabiliana na changamoto za utoaji wa huduma za afya serikali inafanya shughuli zifuatazo.

1. Serikali imetoa jumla ya sh. 2,700,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya afya 6 ili viweze kutoa huduma za upasuaji wa dharura kwa wajawazito. Vituo hivyo ni Lubanda na Ibaba (Ileje), Isansa na Iyula (Mbozi), Mbuyuni (Songwe) na Tunduma ( Mji wa Tunduma), ukarabati na upanuzi wa kituo cha afya cha Tunduma umekamilika, ninawahimiza viongozi wa Halmashauri na wahemiwa Wakuu wa Wilaya kundelea kusimamia kwa karibu upanuzi unaofanyika kwenye vituo vyenu ili kukamilisha kaz hoi kwa wakati.

2. Kuendelea kutoa vibali vya ajira za watumishi wapya ili kuendelea kupunguza pengo la watumishi wa afya. Katika mwaka 2018 , Mwezi huu wa saba Serikali imeajiri watumishi zaidi ya 6,100 nchi nzima ambapo Mkoa wetu umepata watumishi 278 wa kada mbalimbali ambao watapunguza tatizo la upungufu wa watumishi wa afya mkoani kwetu.

3. Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya ununuzi wa dawa, vifaatiba na vitendanishi hadi kufikia sh. **Bilioni 269** kwa mwaka 2017/2018, Mkoa wetu umepangiwa kiasi cha sh. **sh**. **4,291,644,195.00** ambazo zimeongeza upatikana wa dawa katika vituo vya huduma za afya.

4. Serikali inawahimiza viongozi wote wa Halmashauri kuwahamasisha wananchi kushiriki ujenzi wa zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya kwa kila kata, na katika hili ninatoa agizo kwa kila Halmashauri itenge bajeti ya kuanza kujenga angalau kituo kimoja cha Afya kwenye mpango wa mwaka 2018/2019 unaoendelea kuandaliwa.

5. Kuimarisha huduma za kitabibu kwa kuipandisha hadhi Hospitali ya Wilaya ya Mbozi ili itumike kama Hospitali Teule ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe.

**Ndugu washiriki:** Ni matumaini yangu kuwa katika kikao hiki tutaweza kujadili na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta ya afya katika Mkoa wa Songwe ili kuendeleza mafanikio yaliyofikiwa na kuboresha maeneo yenye changamoto ili kuimarisha hali za afya za wananchi wa Mkoa wetu.

Nirudie tena kuwashukuru washiriki/Wadau wote mliojitokeza kwa wingi ili kufanikisha kikao hiki.
Baada ya kusema hayo namalizia kwa kusema tushirikiane kujenga jamii yenye afya, na ustawi bora ili iweze kushiriki kikamilifu kwenye ujenzi wa uchumi wa viwanda. Kikao hiki cha wadau wa Afya katika Mkoa wa Songwe kimefunguliwa Rasmi.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

Mh. Chiku A. Gallawa
**MKUU WA MKOA**
**SONGWE.**